**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI JUHUDI

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**MKUU WA SHULE 0753-477-854**

**SHULE YA SEKONDARI JUHUDI.**

**S.L.P 70342**

**Tarehe ....................................**

**Mzazi/**Mlezi **wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI JUHUDI HALMASHAURI YA JIJI LA DAR-E-SALAAM MKOA WA DAR-ES-SALAAM MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2023** na atasoma tahasusi ya …………
Shule ya Sekondari Juhudi ni ya kutwa ipo katika Manispaa ya jiji la Dar-es-salaam eneo la gongo la mboto jeshini,imepakana na chuo cha Kampala upande kusini,ipo umbali wa Kilometa **mbili** kutoka kituo kikuu cha daladala.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023**
Lipia michango mingine katika akaunti ya shule (**CRDB-NA 0150251322900)**
JINA LA AKAUNTI NI **JUHUDI SECONDARY SCHOOL**.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni **sketi mbili rangi ya Dark blue** kwa Wasichana na **suruali mbili rangi ya dark blue** kwa Wavulana.
ii. Mashati mawili,meupe mikono mifupi.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni **Nyeupe** ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe mpya kwa wasichana na soksi mbili nyeusi kwa wavulana
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta rangi ya dark blue
viii. Tai/Skafu rangi ya suruali/sketi

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari **SITA (6)** counter book quire 4.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Scientific Calculator kwa wanaosoma Tahasusi ya HGE
v. Vifaa vya usafi
**HGE** Analeta **Fyekeo** na **Rek**i
**HGK** Analeta **Jembe** na **ndoo ndogo** yenye mfuniko
HGL Analeta **Fyekeo** na **Mfagio 1** wa ndani
HKL Analeta **mfagio 1** wa **Nje** na **Jembe**

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Kutwa**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;

5) **Unapaswa kurudisha fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu ikiambatanishwa. na viambatanisho A, B, C na D pamoja na cheti cha kuzaliwa, leaving certificate ya kidato cha IV na Result slip (Kila cheti kiwe "Original" na kopiyake)**

6)**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**..

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule:**

**Jina la Mkuu wa Shule : HAPPINESS JACOB PALLANGYO**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ______________________

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0753-477-854**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0716-991-811**
  **Mwandamizi Taaluma 0717-283-802**
- **Mwandamizi Malezi 0716-125-400**

KIAMBATANISHO "A"

## HALMASHAURI YA JIJI LA DAR-ES-SALAAM

## JUHUDI SECONDARY SCHOOL

## FOMU YA KUANDIKISHWA

Picha ya mwanafunzi

**(a) TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la Mwanafunzi……………………………
2. Uraia…………………………………………………
3. Dini…………………………………………………..
4. Tarehe yakuzaliwa…………………………………..
5. Mkoa aliozaliwa……………………………………….
6. Yatima /Siyo yatima …………………………………..
7. Kata unayoishi ………………………………………
8. Umbali kati ya unapoishi na shule ilipo……………………………
9. Shule alizosoma kabla ya kuja shule ya sekondari Juhudi

| JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI/SEKONDARI | TAREHE NA MWAKA ALIOANZA | TAREHEE NA MWAKA ALIOMALIZA |
|---|---|---|---|
| 1. | 1 | 1 | 1 |
| 2. | 2 | 2 | 2 |
| 3. | 3 | 3 | 3 |
| 4. | 4 | 4 | 4 |

**B) YAH: MKATABA WA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI;**

Mimi mwanafunzi......................................................................wa kidato cha ………………………nakubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule ikiwemo kutokushiriki katika namna yoyote ile katika migomo,fujo na makosa ya Jinai.

Sahihi..............................

KIAMBATANISHO "B"

**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR-ES-SALAAM**

**JUHUDI SECONDARY SCHOOL**

## A) TAARIFA YA MZAZI/MLEZI

Picha ya

Mzazi

2. Jina kamili la Mzazi/Mlezi…………………………….....
3. Namba za simu mbili ...............................................
3. Uraia ……………………………………………….......
4. Anuani kamili… ..........................................................
5. Sehemu unayoishi .......................................................
6. Mtaa………………………………………………….....
7. Namba ya nyumba.........................................................
8. Kazi ya mlezi ...................................................................

- Jina la mwajiri na idara .......................................................
- Anuani ………………………….....................................
- Namba Simu………………….........................................

9.Sahihi ya Mzazi / Mlezi………………………….

## B) YAH: AHADI YA MZAZI. KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE:

Mimi...................................................................................mzazi /mleziwa mwanafunzi.......................................................................wa kidato cha ………………………nakubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule ikiwemo yanayohusu kuboresha na kukuza nidhamu na taaluma ya mtoto wangu.

Wa S.L.P……………………………….. Simu Na:……………………………….

Jina la mzazi/Mlezi…………………………………………

**……………………………..**

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi**

**KIAMBATANISHO "C"**

# DAR-ES-SALAAM CITY COUNCIL

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

(TO BE COMPETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER AND RETURNED TO THE HEADMASTER OF JUHUDI SECONDARY SCHOOL)

FROM ……………………………………………………………

Re:…………………………………………………………Age…………………

Please examine the above named student and comment on his health by responding to the following items.

Kindly put a tick in form of either YES or NO.

A. Does the student have problems in connection with.

SIGHT…………………. (i)YES (ii) NO

If YES state …………………………………………………..

HEARING……………….. (i)YES (ii) NO

If YES state …………………………………………………..

SPEECH (i)YES (ii) NO

If YES state …………………………………………………..

T.B……………….. (i)YES (ii) NO

If YES state …………………………………………………..

BLOODPRESSURE……… (i)YES (ii) NO

If YES state …………………………………………………..

ANY PHYSICAL DISABILITY (i)YES (ii) NO

If YES state …………………………………………………..

STOOL………………….. (i)YES (ii) NO

If YES state ........................................................................................................... ANY

OTHER FINDINGS…………………………………………………

B. DOCTOR'S RECOMMENDATION......................................................

| …………………. | …………………… | ………………… |
|---|---|---|
| ***Name and Signature*** | ***Designation*** | ***Station*** |

**KIAMBATANISHO “D”**

**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR-ES-SALAAM**

**JUHUDI SECONDARY SCHOOL**

**TAARIFA ZA MAKAZI ANAPOISHI MWANAFUNZI**

**A) OFISIS YA SERIKALI YA MTAA**

JINA LA MWENYEKITI: ..........................................................................................

SAHIHI YA MWENYEKITI ..........................................................................................

NAMBA YA SIMU YA MWENYEKITI...................................................................

MUHURI WA MWENYEKITI

**B) OFISI YA MJUMBE WA SHINA**

JINA LA MJUMBE WA SHINA:............................................................................................

SAHIHI YA MJUMBE WA SHINA..........................................................................................

NAMBA YA SIMU YA MJUMBE ...........................................................................................

MUHURI WA MJUMBE.